



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



### TAARIFA KWA UMMA

#### UTEUZI WA WABUNGE WANAWAKE WA VITI MAALUM CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO


Tarehe 27 Novemba, 2020

Kuanzia tarehe 26/09/2020 Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikipokea barua kutoka kwa Vyama mbalimbali, barua zenyé mapendekezo ya wanawake Wabunge na Madiwani wa Viti Maalum. Tarehe 26/09/2020 Tume ilipokea barua kutoka Chama cha Mapinduzi, na tarehe 19/11/2020 Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Mapendekezo ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum kwa CHADEMA yaliwasilishwa Tume kwa barua. Mnamo tarehe 20/11/2020 Tume katika kikao chake iliteua Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum kwa kuzingatia matakwa ya Katiba na Sheria.

Kuna taarifa zinasambaa kwenye mitandao kuwa Tume imeteuwa Wabunge wa CHADEMA ambao majina yao hayakuwasilishwa kwa kuzingatia taratibu.

Ifahamike kwamba, Katibu Mkuu wa CHADEMA alimuandikia Mkurugenzi wa Uchaguzi barua yeny kumb. Na. C/HQ/ADM/20/TU/05/141 ya tarehe 19/11/2020 ambayo iliwasilisha orodha ya majina ya wanachama wanaopendekezwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum. Tume ilitumia orodha iliyowasilishwa na CHADEMA kuteua Wabunge wa Viti hivyo. Hivyo, Wabunge Wanawake wa Viti Maalum wa CHADEMA waliteuliwa kwa kuzingatia taratibu zote za kikatiba na kisheria.



Dkt. Wilson Mahera Charles

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**